

Swahili: Introduction to the Refugee Minor Program

## Kiswahili: Utangulizi juu ya Mpango wa Kusaidia Wakimbizi wa Umri Mdogo

Mpango wa Kusaidia Wakimbizi wa Umri Mdogo (Refugee Minor Program, (RMP)) unatoa msaada kwa watoto na vijana ambao ni wakimbizi, chini ya miaka 18 ya kuzaliwa na wako Victoria bika kuwa na wazazi. Wanajulikana kama 'Watoto wa kikimbizi wasio na walezi' ('Unaccompanied Humanitarian, or Refugee, Minors', (UHM's)). Wizara ya Uhamiaji na Uraia (Department of Immigration and Citizenship, (DIAC)) inaamua kuwatuma wateja wa UHM wanaoishi Victoria kwenda kwenye RMP.

Kuna aina tatu ya watumiaji wa huduma ya UHM:

- **Wasio na bodi (Non-wards)** ni wale walioko hapa wakiwa na ndugu wa karibu mwenye miaka zaidi ya 21 ya kuzaliwa, ambaye yuko tayari kukubali majukumu ya kuwalea. DIAC itamuomba ndugu huyo kuweka saini ya 'kukubali kulea'.
- **Bodi (Wards)** ni wale wasio na ndugu wa karibu (mwenye miaka zaidi ya 21 ya kuzaliwa) nchini Australia ambaye yuko tayari kukubali majukumu ya kuwalea. Waziri wa Uhamiaji anakuwa ndiye Mlezi wa Kisheria wa kulea huyo mtoto, na anaomba Wizara ya Huduma za Jamii (Department of Human Services, (DHS)), (kupitia RMP) kuhusika kama mlezi aliyechaguliwa (rejea kipengere cha 5(1) cha *Ulezi wa Watoto wa Wizara ya Uhamiaji* (sheria ya IGOC)).
- **Watoto wasio na walezi wanaotafuta ukimbizi** ni watoto na vijana chini ya miaka 18 wanaoingia Australia bila kuwa na wazazi au familia na bila kuwa na idhini kutoka kwenye mamlanka ya Australia na kuomba kutambuliwa kama wakimbizi chini ya haki ya ukimbizi. Wanaweza wasiwe na viza inayokubalika na wanaweza kutambuliwa Kwa kwenye kwenye 'Kizuizi cha kwenye jamii' au 'Kizuizi mbadala' au wanaweza kuwa na viza za mda mfupi.

Tarehe 13 Juni 2008 *Ujumbe wa Uhamiaji wa 2008 (Ulezi wa Watoto)* (mwongozo wa ujumbe) uliweza kurudiwa na kuwekewa saini na Waziri wa Uhamiaji, ambao unaruhusu Ulezi wa Watoto wanaotafuta Ukimbizi usimamiwe na mikoa na Wilaya. Hii inatoa ujumbe kwa Ulezi wa Serikali Kuu kuhusu watoto wanaotafuta ukimbizi bila walezi (pale wanapotambuliwa kama pweke) kusaidiwa na RMP.

Kazi ya RMP katika mazingira hayo inahitaji uangalizi wa uangalifu na majadiliano na DIAC, na yanaweza kujumuisha kutafuta, kupima na kuchagua mlezi anayestahili, kutoa taarifa na maoni kwenda DIAC kama matokeo ya uchunguzi ili wafanye maamuzi; na kufanya kazi pamoja na walezi na watoto/vijana.